JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

**HOTUBA YA MGENI RASMI, MHE. MHANDISI EVARIST NDIKILO**
**MKUU WA MKOA WA PWANI**
**KATIKA UFUNGUZI WA MAFUNZO YA WADADISI WA SENSA YA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI YA MWAKA WA KILIMO 2019/20 KWA KANDA YA PWANI KATIKA UKUMBI WA CHUO CHA UUGUZI BAGAMOYO, MKOA WA PWANI**

**TAREHE 27 JULAI, 2020**

**Mwakilishi wa Mtakwimu Mkuu wa Serikali;**
**Viongozi kutoka Ofisi ya Taifa ya Takwimu;**
**Meneja wa Takwimu Mkoa wa Dar es Salaam, Pwani, Lindi na Mtwara;**
**Maafisa Kilimo kutoka ngazi ya Mkoa na Halmashauri;**
**Washiriki wa Mafunzo/Wadadisi;**
**Ndugu Waandishi wa Habari;**
**Mabibi na Mabwana,**

**Aslam Alekum/ Tumsifu Yesu Kristu!**

**Ndugu Washiriki,**

Kwanza kabisa, hatuna budi kumshukuru Mwenyezi Mungu **Mwingi wa Rehema na Utukufu**, kwa kutujalia uzima na afya njema na kutuwezesha kukutana hapa siku ya leo kwa ajili ya ufunguzi wa Mafunzo ya Wadadisi wa Sensa ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi ya Mwaka wa kilimo 2019/20. Pili, napenda kutumia fursa hii kuushukuru Uongozi wa Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS) chini ya uongozi wa Mtakwimu Mkuu wa Serikali Dkt. Albina Chuwa kwa kunipa heshima hii ya kuwa Mgeni Rasmi katika hafla hii muhimu na adhimu ya uzinduzi wa mafunzo haya katika kanda yetu. Aidha, nawashukuru viongozi wenzangu na watendaji wa mkoa mlioungana nami hapa kushuhudia uzinduzi huu. **Nyote ninawashukuru sana.**

**Ndugu Washiriki,**

Ni ukweli usiopingika kuwa kilimo ni uti wa mgongo wa uchumi na maisha yetu hapa nchini. Tanzania ina watu wenye uwezo wa kufanya kazi zaidi ya asilimia 60 wanaotegemea kilimo kuendeleza maisha yao. Aidha, Sekta ya Kilimo ndiyo inayotupatia mahitaji yetu muhimu ya chakula kwa wananchi waishio mijini na vijijini lakini pia jitihada za Serikali yetu katika ujenzi wa uchumi wa viwanda zinategemea sana maendeleo na ufanisi wa sekta ya kilimo. Sekta ya Kilimo isipofanya vizuri inaathiri wananchi wote, hivyo kilimo ni sekta yetu ya msingi.

**Ndugu Washiriki,**

Kufanyika kwa Sensa ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi ni zoezi lenye umuhimu wa kipekee kwa kuwa ina lengo la kufahamu hali halisi ya ***kilimo chetu, ufugaji wetu na shughuli zetu za uvuvi***. Takwimu zitakazokusanywa zitaonesha hali halisi ya sekta hii nchini na kuiwezesha Serikali kupanga Sera, Mipango na Programu mbalimbali za kuendelea, kuimarisha uchumi na kuboresha hali ya maisha ya wananchi. Aidha, takwimu hizo zitatumika kufuatilia na kutathmini utekelezaji wa Sera, Mipango na Programu mbalimbali za sekta ya kilimo. Vile vile, takwimu hizi zitatumika kufuatilia viashiria vya **Malengo Endelevu ya Maendeleo ya Mwaka 2030** hususani kwenye lengo ***Namba Mbili la Kutokomeza Njaa, Kuwa na Uhakika wa Chakula, Lishe Bora na Kukuza Kilimo*****; Ajenda ya Maendeleo ya Afrika ya mwaka 2060 na Dira ya Maendeleo ya Afrika Mashariki ya Mwaka 2050.** Hivyo, kila mmoja wetu kuanzia wananchi hadi viongozi wa juu katika mikoa yetu tuna jukumu la kuipa uzito Sensa hii kwa kuhakikisha inafanyika kwa ufanisi ili itoe matokeo tarajiwa.

**Ndugu Washiriki,**

Nimeeleza kwa ujumla umuhimu wa kilimo na sasa naona ni vyema kuonesha kwa takwimu namna Kilimo kilivyo muhimu katika uchumi na maendeleo ya nchi yetu. Mathalan, mwaka 2019, sekta ya kilimo ilichangia katika Pato la Taifa kwa asilimia 26.6 na kwa upande wa mauzo ya nje asilimia 24.3 ya fedha za kigeni zilizopatikana zilitokana na mazao ya kilimo. Tafsiri ya takwimu hizi ni kuwa, kwa mwaka huo wakulima tulizalisha zaidi, tukavuna zaidi na tukauza zaidi. Wafugaji tulifuga zaidi, tukauza zaidi na wavuvi ndio hivyo hivyo. Kwa hiyo, hatuna budi sisi tulio katika sekta ya kilimo kujivunia mchango wetu huu kwa sababu tumechangia na tunaendelea kuchangia katika maendeleo tunayoyaona hivi sasa. Tumesikia Mheshimiwa Rais wa Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. John Pombe Magufuli akisema tunatumia fedha za ndani kujenga karibu miradi yetu yote mikubwa ya kimkakati. Miradi hiyo ni pamoja na Reli ya Kisasa, miradi ya nishati, ununuzi wa ndege na miundombinu ya barabara. Maana yake ni kuwa sisi wakulima, wafugaji na wavuvi wa kanda yetu hii yenye mikoa ya Dar es Salaam, Pwani, Lindi na Mtwara, tunachangia sehemu kubwa ya ujenzi wa miradi hiyo. Jambo hili ni la kujivuania sana, kwa kuwa tunajenga nchi yetu na kudhihirisha ule usemi wa ***uhuru na kazi na mjenga nchi ni mwananchi mwenyewe***. Ndio maana kwa kutambua mchango mkubwa wa sekta hii, Serikali inafanya Sensa kila baada ya miaka mitano na pia kila mwaka hufanya tafiti mbalimbali ambazo husaidia kupata takwimu muhimu za kuendeleza sekta hii.

**Ndugu Washiriki,**

Kama alivyoeleza hapo awali Mwakilishi wa Mtakwimu Mkuu wa Serikali, mafunzo haya yatakuwa na sehemu mbili za Nadharia na Vitendo. Nadharia itahusu namna ya kujaza Dodoso la Wakulima Wadogo; Dodoso la Mashamba Makubwa; Dodoso la Jamii; Mbinu za Udadisi; kutumia teknolojia mpya katika kukusanya taarifa yaani matumizi ya VISHIKWAMBI (***tablets***) na hatimaye yatakamilishwa kwa kufanya mtihani. Kuhusu sehemu ya pili ya vitendo, nimefurahi kusikia kuwa waandaaji wa mafunzo haya wamelizingatia hili kwa kuwa Sensa si zoezi la kubahatisha kwa sababu kukosa kuoanisha nadharia na vitendo kunaweza kuleta athari kubwa katika utendaji wenu na ikitokea hivyo kunaweza kuathiri pia matokeo ya Sensa, jambo ambalo hatulitarajii. Katika mnasaba huo, ningependa kutoa wito kwenu nyote washiriki kuhakikisha mnafuatilia kwa makini mafunzo haya hatua kwa hatua na kwa wakufunzi kufuatilia mwenendo wa wanafunzi wenu ili kuhakikisha wanapata kile wanachopaswa kujifunza kwa faida ya malengo ya Sensa hii.

Naamini washiriki mmejiandaa vyema na niseme hii ni fursa nzuri kwenu kushiriki katika mafunzo haya yakiwa ni sehemu ya utekelezaji wa Sensa ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi kwa sababu mnaongeza ujuzi na mtapata fursa ya kujifunza zaidi juu ya maisha ya watu wetu na jamii yetu. Naamini baada ya Sensa hii mtakuwa na upeo mpana siyo tu kwa Sekta ya Kilimo na namna jamii zinavyoishi na kufanya shughuli zao kuendesha maisha bali pia mnaweza kuvutiwa hatimaye kuamua kuwekeza katika sekta hii kwani ndiyo sekta yenye uwezo mkubwa wa kutimiza lengo la kuleta maendeleo jumuishi nchini.

Nasaha yangu kwenu vijana pamoja na kuzingatia vigezo na masharti ya jukumu la kutekeleza Sensa, lakini jambo jingine muhimu ambalo ndilo litakalofanikisha jukumu lenu hilo ni kuzingatia nidhamu kwa jumla wakati wote mtakapokuwa huko mkikusanya taarifa. Mfahamu kwamba mkiwa katika utekelezaji wa majukumu yenu ya Sensa huko mmetumwa na Serikali. Maana yake mnaiwakilisha Serikali, hivyo lazima muoneshe taswira ya Serikali kwa wananchi wote mtakaokutana nao. Naamini kuwa wakati wa mafunzo hili litafafanuliwa zaidi. Hata hivyo, ninawaona ninyi ni vijana wazuri, wazalendo na wachapakazi hivyo hamtaiangusha Serikali yenu ambayo imejizatiti kuwaletea maendeleo kwa haraka ikiwemo katika sekta hii ya Kilimo.

**Ndugu Washiriki,**

Wakati tukielekea kwenye Sensa ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi ya mwaka 2019/20, sina budi kuwakumbusha na kusisitiza kuwa mafanikio niliyoyataja hapo awali yanatokana na matumizi ya matokeo ya Sensa ya mwaka 2007/08 ambayo ilifanyika kwa ufanisi mkubwa. Takwimu zilionesha maeneo yaliyofanikiwa na kupiga hatua kubwa, maeneo yaliyosogea kidogo, maeneo yenye changamoto nyingi na maeneo ambayo hayakupiga hatua kabisa. Mipango na Sera ambazo tumekuwa tukizitekeleza na ambazo zimetuletea mafanikio niliyoyataja zilitumia takwimu za Sensa ya mwaka 2007/08. Kwa hiyo, ni dhahiri kuwa ili tuendelee kupiga hatua zaidi na zaidi katika kuimarisha kilimo, mifugo na uvuvi, hatuna budi sote kushiriki katika Sensa kikamilifu bila ajizi.  Kwa upande wa viongozi kuanzia ngazi ya mkoa hadi kitongoji/mtaa tuhakikishe kuwa tunatimiza wajibu wetu ambao kwanza ni

kuhakikisha mazingira ya utekelezaji wa Sensa hii yanaimarishwa kwa kuwaelimisha wananchi umuhimu wa Sensa hii.

**Ndugu Washiriki,**

Kuanzia sasa tunapoitisha vikao vyetu tuhakikishe kuwa ujumbe wa Sensa uwe ni wa kudumu na katika mikutano yetu na wananchi tuwaelimishe na kuwahimiza kutoa ushirikiano kwa wadadisi wakati wote wa zoezi hili linapofanyika. Kwa upande wa wananchi wajibu wao mkubwa ni kushirikiana na wadadisi kwa kujibu maswali kwa usahihi na ufasaha bila ya kuficha ukweli wa taarifa. Wananchi wanapojibu maswali kwa usahihi maana yake siyo tu kuwa wanachangia katika uzalishaji wa takwkimu bora lakini wanajihakikishia maendeleo yao wenyewe. Hata hivyo, ningependa kuwakumbusha wananchi kuwa Sheria ya Takwimu Sura 351 inawataka wananchi kushirikiana na NBS au Wawakilishi wao wakati wote wa zoezi la kukusanya Takwimu na kushindwa kufanya hivyo watakuwa wametenda kosa na wanaweza kuchukuliwa hatua kwa mujibu wa sheria. Wananchi watakaohojiwa hawana haja ya kuwa na hofu juu ya majibu wanayoyatoa kwa kuwa kwa mujibu wa Sheria hiyo, taarifa watakazozitoa zitakuwa ni siri na zitatumika kwa ajili ya masuala ya kitakwimu tu. Wako wanaodhani taarifa hizo zitazokusanywa zitatumika kuwakadiria kiwango cha kutozwa kodi hilo nalo si kweli bali lengo muhimu la Sensa hii ni kutaka kuimarisha na kuboresha Sekta yetu ya Kilimo ili iweze kuzalisha zaidi na kuongeza Pato la Taifa, pato la wastani la mwananchi na hatimaye kuchangia katika kupunguza kiwango cha umasikini nchini.

**Ndugu Washiriki,**

Mwisho lakini siyo kwa umuhimu, sote tunafahamu kuwa bado Dunia ipo katika hatari ya maambukizi ya virusi vya Corona (COVID-19) ambavyo husababisha ugonjwa wa Homa Kali ya Mapafu. Hivyo, hatuna budi wakati wote tutakapokuwa katika utekelezaji wa jukumu letu hili la Sensa ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi kuchukua tahadhari zote zilizotolewa na Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto za namna ya kujikinga dhidi ya maambukizi ya virusi hivi.

***Ndugu viongozi na watendaji wa Serikali, washiriki wa mafunzo,*** baada ya kusema hayo, **NAPENDA KUTAMKA KWAMBA**, **MAFUNZO YA WADADISI WA SENSA YA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI YA MWAKA WA KILIMO 2019/20, KANDA YA MASHARIKI YAMEFUNGULIWA RASMI.**

**ASANTENI KWA KUNISIKILIZA.**